# SHIRIKISHO LA JUMUIYA ZA WANAFUNZI WATANZANIA KATIKA JAMHURI YA WATU WA CHINA (TASAFIC)

**KANUNI ZA SHIRIKISHO LA JUMUIYA ZA WANAFUNZI WATANZANIA**

**NCHINI CHINA**

**(TANZANIA STUDENTS ASSOCIATIONS' FEDERATION IN CHINA - TASAFIC)**

2019 (Marekebisho 2021 & 2025)

**Toleoe la 2025**

# UTANGULIZI

Shirikisho la Jumuiya za Wanafunzi Watanzania katika Jamhuri ya Watu wa China ni chombo kinachowaunganisha wanafunzi wote Watanzania wanaosoma kwenye taasisi za elimu katika Jamhuri ya Watu wa China kupitia Jumuiya zao zilizopo kwenye majimbo, miji au vyuo. Shabaha ya kuundwa kwa Shirikisho hili ni kwa ajili ya kushiriki kutatua changamoto za kielimu za wanavyuo na kuwaandaa kuwa wasomi wenye kuwajibika ipasavyo na kuwa raia wema wa Taifa letu. Pia chombo hiki ni sawa na tanuri la chuma la kuokea wasomi wazuri na bora wenye kujitambua. Kwa hivyo, Shirikisho la Jumuiya za Wanafunzi Watanzania katika Jamhuri ya Watu wa China tunatambua kuwa kuunganisha fikra za pamoja za wasomi kutachochea harakati za kuleta mapinduzi ya kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia na kujenga jamii ya watu iliyo sawa nchini Tanzania kwa kutumia elimu na maarifa tunayoyapata. Ili kufanikisha haya tunahitaji chombo madhubuti kinachounganisha fikra na vitendo vya wanafunzi waliopo katika Jamhuri ya Watu wa China. Shirikisho la Jumuiya za wanafunzi Watanzania katika Jamhuri ya Watu wa China litatekeleza malengo na madhumuni yake kupitia utaratibu makhsusi lililojiwekea kwa misingi ya udugu, usawa, uwajibikaji na ushirikishwaji katika kushiriki kikamilifu kusaidiana kuijenga na kuitangaza nchi yetu na rasilimali zake kupitia fursa ya elimu tunayoipata. Shirikisho la Jumuiya za wanafunzi Watanzania katika Jamhuri ya Watu wa China tutaratibu na kukuza uhusiano na ushirikiano baina yake na taasisi zinazojishughulisha na elimu, sayansi, utamaduni na ajira katika Jamhuri ya Watu wa China na Tanzania. Tunazingatia kwamba elimu ndiyo rasilimali kuu ya Taifa letu, pia tunakubali kimsingi kwamba ili tuweze kupata elimu bora, wanafunzi tunalazimika kuwa na nidhamu na silka ya uchunguzaji ili kupata uelewa mpana wenye kuyafahamu mazingira tuliyopo.

Imesainiwa Na:

| | |
|---|---|
| ________________(Tarehe 10/06/2025) | ________________(Tarehe____/___/_____) |
| Jivitius Ching'oro Sabatho | Mhe. Balozi. Khamis Mussa Omar |
| Mwenyekiti wa TASAFIC 2024/2025 | Balozi wa Tanzania Nchini China Mlezi wa TASAFIC |

# MPANGILIO WA VIFUNGU


## SEHEMU YA KWANZA: MASHARTI YA AWALI

1. Ufupisho wa jina la Shirikisho
2. Anwani ya Shirikisho
3. Kauli ya Shirikisho
4. Ufafanuzi wa maneno

## SEHEMU YA PILIL: MADHUMUNI NA MAJUKUMU YA SHIRIKISHO

5. Madhumuni na majukumu ya Shirikisho

## SEHEMU YA TATU: UANACHAMA

6. Jumuiya kuwa Mwanachama
7. Jumuiya hai
8. Ada ya mwanachama
9. Maombi ya Jumuiya kuwa mwanachama
10. Haki za Jumuiya
11. Wajibu wa Jumuiya
12. Ukomo wa Jumuiya
13. Jumuiya kujitoa katika Shirikisho

## SEHEMU YA NNE: UONGOZI

14. Uongozi wa Jumuiya Mwanachama
15. Uongozi wa Shirikisho
16. Utaratibu wa upatikanaji wa viongozi
17. Sifa za Kiongozi
18. Miiko ya Kiongozi
19. Ukomo wa Uongozi
20. Viongozi Wakuu wa Shirikisho
21. Mwenyekiti wa Shirikisho
22. Makamu Mwenyekiti wa Shirikisho
23. Katibu Mkuu wa Shirikisho
24. Naibu Katibu Mkuu wa Shirikisho
25. Mweka Hazina wa Shirikisho
26. Njia za Upatikanaji wa Viongozi wa Shirikisho
27. Mlezi wa Shirikisho

## SEHEMU YA TANO: VIKAO, KURUGENZI NA KAMATI ZA SHIRIKISHO

28. Vikao vya Shirikisho
29. Mkutano Mkuu wa Shirikisho
30. Kazi na Uwezo wa Mkutano Mkuu
31. Vikao vya Mkutano Mkuu
32. Akidi ya Vikao vya Mkutano Mkuu

33. Maamuzi ya vikao
34. Halmashauri Kuu ya Shirikisho
35. Kazi na Uwezo wa Halmashauri Kuu
36. Vikao vya Halmashauri Kuu
37. Kamati Tendaji ya Shirikisho
38. Kazi za Kamati Tendaji
39. Vikao vya Kamati Tendaji
40. Sekretarieti ya Shirikisho
41. Kazi za Sekretariet ya Shirikisho
42. Vikao vya Sekretarieti
43. Kurugenzi na kamati za Shirikisho
44. Kurugenzi ya Uchumi na Fedha
45. Kazi za Kurugenzi
46. Kamati za Shirikisho

**SEHEMU YA SITA: MFUKO WA SHIRIKISHO**

47. Mfuko wa Shirikisho na Utaratibu wa Matumizi
48. Usimamizi wa Mfuko

**SEHEMU YA SABA: VYANZO NA USIMAMIZI WA MAPATO**

49. Vyanzo vya Mapato ya Shirikisho
50. Usimamizi wa Mapato ya Shirikisho
51. Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Shirikisho

**SEHEMU YA NANE: MASHARTI MAALUMU**

52. Akidi za Vikao
53. Ufikiwaji wa Maamuzi
54. Lugha ya Mikutano

**SEHEMU YA TISA: UKOMO WA SHIRIKISHO**

55. Sababu za Ukomo wa Shirikisho
56. Hatua baada ya Kukoma kwa Shirikisho

**SEHEMU YA KUMI: MAKOSA NA ADHABU**

57. Makosa ya Udanganyifu na Kutoa Taarifa za Uongo
58. Makosa ya Matumizi Mabaya ya Fedha

**SEHEMU YA KUMI NA MOJA: MAREKEBISHO YA KANUNI**

59. Idhini ya Marekebisho ya Kanuni
60. Marekebisho ya Kanuni za Katiba hii

## SEHEMU YA KWANZA: MASHARTI YA AWALI

### 1. Ufupisho wa jina la Shirikisho

i. Jina la Shirikisho litakuwa “Shirikisho la Jumuiya za wanafunzi Watanzania katika Jamhuri ya Watu wa China, kwa Kiingereza Tanzania Students Associations’ Federation in China.

ii. Kifupi cha Shirikisho ni ‘TASAFIC’.

iii. Makao Makuu ya Shirikisho yatakuwa mahali Ubalozi wa Tanzania ulipo katika Jamhuri ya Watu wa China.

### 2. Anuani ya Shirikisho

Anuani ya Shirikisho itakuwa kama ifuatavyo:

Ibara ya 3 Anuani ya Shirikisho itakuwa: - Tanzania Students Associations’ Federation in Chinac/o. Tanzania Embassy in Beijing 8 LiangMa He Nan Lu, Sanlitun, 100600 Beijing, P.R. CHINA

| | |
|---|---|
| Email: | tasafictc@gmail.com |
| Instagram: | tasafic |
| Whatsapp Channel: | Fursa za Masomo China |
| X(Twitter): | tasafic |
| Facebook: | Tasafic China |
| Youtube: | tasafic |
| Website: | http://tasafic.com |

### 3. Kauli ya Shirikisho

Kauli ya Shirikisho ni “Elimu na Umoja Tuijenge Tanzania”.

### 4. Ufafanuzi wa Maneno

Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vinginevyo:

“Ada” maana yake ni kiasi cha fedha kinachotolewa na Jumuiya mwanachama kama mchango wake wakila mwaka kwa Shirikisho;

“Anuani” maana yake ni sehemu na mawasiliano ya Makao Makuu ya Shirikisho ambayo kwa mujibu wa Kanuni hizi yatakuwa ni katika ofisi za Ubalozi;

“Cheti” maana yake ni alama ya utambulisho anayopewa mwanashirikisho kutambua mchangowake katika jumuiya/shirikisho;

“Jumuiya” maana yake ni Chama au Umoja wa wanafunzi Watanzania kwenye majimbo, vyuo au miji;

“Jarida” maana yake ni makala iliyoandikwa na Kamati ya Jarida ikijumuisha pamoja matukio mbalimbali yaliyokusanywa kutoka kwa Jumuiya mbalimbali kwa lengo la kuendelea kuhabarisha Watanzania walioko China na nchini Tanzania;

“Kanuni” maana yake ni miongozo ya Shirikisho za mwaka 2014/2019/202 pamoja na marekebishoyake ya mwaka 2025;

“Kamati Maalumu” maana yake ni kamati zenye jukumu maalumu ambazo huteuliwa naMwenyekiti wa kamati tendaji;

“Kamati ya Ushauri” maana yake ni kamati inayoundwa na viongozi wastaafu (kamati tendaji)kwa lengo la kumshauri Mwenyekiti wa Kamati tendaji;

“Kanzidata” maana yake ni orodha ya majina ya wanafunzi wa Kitanzania ambao wanaunda Shirikisho kupitia Jumuiya zao;

“Katibu Mkuu” maana yake ni Mtendaji Mkuu wa Shirikisho kama ilivyoelezwa katika Kanuni hizi;

“Kurugenzi” maana yake ni Idara kuu yoyote ya Shirikisho kama inavyoelezwa ndani ya Kanuni hizi;

“Mali” zitajumuisha nyaraka, fedha, na rasilimali zote zinazohamishika na zisizohamishika zilizochini ya Shirikisho;

“Makamu Mwenyekiti” maana yake ni Mwenyekiti msaidizi wa Shirkisho kama ilivyoelezwa ndani ya Kanuni hizi;

“Mlezi” maana yake ni msimamizi wa Shirikisho kama inavyoelezwa katika kanuni hizi;

“Mweka Hazina” maana yake ni msimamizi na mtunzaji wa fedha za Shirikisho kama inavyoelezwa ndani ya Kanuni hizi;

“Mwenyekiti” maana yake ni kiongozi wa juu na msemaji wa Shirikisho kama inavyoelezwa katika kanuni hizi;

“Naibu Katibu Mkuu” maana yake ni Mtendaji mkuu msaidizi wa Shirikisho kama inavyoelezwandani ya Kanuni hizi;

“Taarifa rasmi” maana yake ni maelezo ya kina yatakayotolewa na Shirikisho na jumuiya mwanachama kwa njia ya maandishi au njia nyingine ya mawasiliano juu ya mambo yanayohusu Shirikisho;

“Shirikisho” maana yake ni Umoja wa Jumuiya za wanafunzi Watanzania katika Jamhuri ya Watu wa China, na itakuwa na maana sawa na Tanzania Students Associations’ Federation in China, kwa kifupi TASAFIC;

“Taarifa rasmi” maana yake ni maelezo ya kina yatakayotolewa na Shirikisho na jumuiya mwanachama kwa njia ya maandishi au njia nyingine ya mawasiliano juu ya mambo yanayohusu Shirikisho;

“Tuzo” maana yake ni zawadi anayopewa mwanajumuiya baada ya kufikia lengo lenye manufaa kwa shirikisho;

“Ubalozi” maana yake ni Ubalozi wa Tanzania katika Jamhuri ya Watu wa China;

“Uchaguzi” maana yake ni utaratibu wa kuwapata viongozi wakuu wa Shirikisho;

“Vikao” maana yake ni mikutano yote ya Shirikisho inayofanyika na kutambuliwa na kanuni hizi;

“Zawadi” maana yake ni shukrani anayopewa mwanajumuiya baada ya kufikia lengo lenye manufaa kwa shirikisho;

## SEHEMU YA PILI: MADHUMUNI NA MAJUKUMU YA SHIRIKISHO

### 5. Madhumuni na Majukumu ya Shirikisho

Madhumuni na Majukumu ya Shirikisho yatakuwa yafuatayo:-

i. Kuwapokea na kuwaongoza wanafunzi wa kitanzania wanaofika nchini China kwa mara ya kwanza kupitia Jumuiya za miji wanayoenda kusoma.

ii. Kuwaunganisha wanafunzi Watanzania wanaosoma na kuishi katika Jamhuri ya Watu wa China.

iii. Kuratibu masuala ya kielimu ya wanafunzi kupitia Jumuiya zilizopo majimboni.

iv. Kuwa kiungo kwa ajili ya kuratibu masuala ya kielimu ya wanafunzi kupitia Jumuiya zilizopo majimboni na Ubalozi.

v. Kusimamia na kushirikiana na Jumuiya wanachama katika shughuli mbalimbali za kijamii zinazowahusu wanajumuiya.

vi. Kusambaza taarifa za fursa mbalimbali kwa Watanzania wote ikiwa ni pamoja na ufadhili wa masomo na ajira nchini Tanzania na China.

vii. Kuwa kiungo kwa serikali za Tanzania na China kwa kupitia Ubalozi na Wanafunzi waishio katika Jamhuri ya Watu wa China.

viii. Kuwasilisha na kutetea maslahi na haki za wanafunzi wa kitanzania walioko masomonikatika Jamhuri ya Watu wa China.

ix. Kushiriki kikamilifu katika fursa zenye kuitangaza Tanzania na rasilimali zake katika Jamhuri ya Watu wa China.

x. Kushiriki katika mikutano, midahalo na makongamano ili kuwajengea wanajumuiyauwezo katika masomo yao.

xi. Kuwajenga wanajumuiya katika maadili ya uzalendo, umoja na utaifa.

xii. Kushirikiana na Ubalozi wa Tanzania uliopo Jamhuri ya watu wa China kuwatafutia wanafunzi mafunzo ya muda mfupi na mazoezi ya vitendo ili kukuza kiwango chao cha elimu na kuwajengea uwezo zaidi.

xiii. Kuwa chemchem ya fikra na mawazo ya kimaendeleo kwa Taifa.

xiv. Kufanya tafiti za changamoto zinazolikabili Taifa.

xv. Kushirikiana na Watanzania waliowahi kusoma katika Jamhuri ya Watu wa China kutengeneza fursa zaidi za kielimu na ushauri kwa Serikali ya Tanzania.

xvi. Kushirikiana na Ubalozi kuwaunganisha wanashirikisho na watanzania kwa ujumla na viongozi

kutoka serikalini, asasi za kiraia, mashirika, makampuni na wageni mbalimbali wanaotembelea Jamhuri ya Watu wa China.

xvii. Kuteua wahudumu na wafanyakazi wa muda ndani ya Shirikisho ambao watafanya kazi maalumu na kuwalipa inapobidi.

xviii. Kutengua uteuzi wa wahudumu na wafanyakazi wa muda ndani ya Shirikisho ambao watafanya kazi maalumu na kusitisha malipo inapobidi.

xix. Kuchapisha vipeperushi au nyaraka zingine au kutangaza na chombo chochote ndani ya Shirikisho ikiwa ni pamoja na media za elektroniki wakati Kamati ya tendaji na Timu ya Uongozi inavyofikiria kutangaza malengo ya Shirikisho.

xx. Kukusanya pesa kwa usajili wa Jumuiya wanachama na njia nyingine yoyote kadri inavyoweza kutoka wakati kwa muda kupitishwa na kamati tendaji ndani ya sheria inayoongoza mwenendo wa jumuiya. Fedha hizo zinapaswa kutumiwa kufanikisha malengo ya Shirikisho;

xxi. Kukubali zawadi, wasia au kifaa au mali halisi au ya kibinafsi iwe chini ya uaminifu maalum kwa maridhiano na Halmashauri Kuu;

xxii. Kuwasiliana na idara za serikali na mashirika mengine husika na wakala ili kuendeleza malengo ya Shirikisho bila kujihusisha na chama chochote cha kisiasa.

xxiii. Kuwa sehemu ya utatuzi wa changamoto za wanafunzi watanzania.

xxiv. Kuwa kiungo cha wanafunzi na wanadiaspora wengine ndani na nje ya china.

**NB:**

a) Taarifa za Viongozi wa Jumuiya ama wahusika wa mapokezi ya wanafunzi zitapaswa kuwepo Ubalozi wa Jamhuri ya Watu wa China nchini Tanzania ili wanafunzi wapewe taarifa hizo pale tu wanapoenda kuchukua viza zao.

b) Kuwepo na link ya taarifa za wanafunzi na majimbo watakayokuwepo na wajaze moja kwa moja kwenye kanzidata pindi waingiapo nchi ya Jamhuri ya Watu wa China.

c) Kukiwa na mwanajumuiya ambaye ameugua kwa muda mrefu, viongozi wa Jumuiya husika wawasiliane na Kamati Tendaji ya Shirikisho na kuona namna nzuri ya kumhudumia mwanajumuiya huyo ikizingatia kigezo cha uhai wa Jumuiya hiyo.

d) Endapo mwanajumuiya atafariki, Shirikisho litapaswa kushiriki kwa kutoa rambirambi na kutembelea wafiwa au kutuma wawakilishi inapowezekana.

## SEHEMU YA TATU: UANACHAMA

### 6. Jumuiya kuwa Mwanachama

i. Jumuiya ya Wanafunzi Watanzania walio katika mji au jimbo lolote katika Jamhuri ya watu wa China inapaswa kuwa mwanachama wa Shirikisho.

ii. Ili kutambulika kuwa mwanachama wa Shirikisho, Jumuiya italazimika kuwa na idadi ya wanachama wasiopungua watatu.

iii. Endapo Jumuiya haitafikisha idadi ya wanachama watatu, Jumuiya hiyo italazimika kujiunga na jumuiya nyingine ya jimbo la jirani endapo mazingira ni rafiki.

iv. Watanzania wasiokuwa na Jumuiya na wala Jumuiya karibu watawajibika moja kwa moja kwa Kamati Tendaji kwa utaratibu wa ada maalumu ya Shirikisho na itakayoridhiwa na Halmashauri Kuu.

v. Jumuiya inayohitaji kujiunga na Shirikisho itatakiwa kuandika barua kwa Halmashauri Kuu.

vi. Jumuiya itapaswa kutii na kuheshimu maamuzi rasmi ya vikao kuanzia ngazi ya Kamati Tendaji, Halmashauri Kuu na Mkutano Mkuu.

### 7. Jumuiya hai

i. Jumuiya itatambulika kuwa jumuiya hai kwa kuchangia ada, michango na kushiriki shughuli mbalimbali za Shirikisho kama ilivyoainishwa katika Kanuni hizi.

ii. Viongozi wake kushiriki vikao halali vya shirikisho

iii. Viongozi wake kuwepo kwenye makundi sogozi ya idara husika kwa mujibu wa vyeovyao

iv. Kwa mujibu wa kanuni ya 9-iv, Jumuiya itakaposhindwa kulipa ada hiyo itawekwa chini ya uangalizi kwa siku saba

v. Kwa mujibu wa kanuni ya 7-iv, Jumuiya ikishindwa itaondolewa mpaka paleitakapokuwa tayari kukidhi vigezo.

**8. Ada ya mwanachama**

i. Jumuiya mwanachama itachangia ada kama itakavyoainishwa na Halmashauri Kuu na kuwasilishwa kwa Mhazini wa Shirikisho kwa ajili ya mfuko na uendeshaji wa Shirikisho.

ii. Jumuiya italipa ada yake ya uanachama kwa mwaka kulingana na idadi ya wanachama wake kama ifuatavyo: wanachama 3-10 = yuan 100; wanachama 11-25 = yuan 250;

iii. wanachama 26-50 = yuan 500; wanachama 51-100 = yuan 750; na wanachama zaidi ya 100 = yuan 1000

iv. Mwaka wa Fedha wa shirikishoni utaenda sambamba na uchaguzi mkuu wa TASAFIC yaani utaanza Julai na kuisha Juni mwaka unaofuata.

v. Kila Jumuiya inapaswa kulipa ada ya mwaka kwa mkupuo mmoja au kwa miezi sita na ssi pungufu ya hapo

vi. Viongozi wanapaswa kulibeba suala la ada wao kwanza kabla ya kwenda kwa wanajumuiya.

vii. Ada za wanajumuiya ndani ya Jumuiya mwanachama zitaamuliwa na uongozi wa Jumuiya husika kulingana na mazingira ya Jumuiya mama.

viii. Kiwango cha ada kinaweza kubadilika kulingana na wakati na hali ya Jumuiya baada ya kupitishwa na Halmashauri Kuu pale itakapohitajika.

**9. Maombi ya Jumuiya kuwa mwanachama**

i. Ili kujiunga na Shirikisho, jumuiya husika itawasilisha ombi lake kwa Kamati Tendaji kwa njia ya maandishi.

ii. Kamati Tendaji kwa kushirikiana na Halmashauri Kuu itatoa maamuzi ndani ya muda usiozidi siku 21 za kazi baada ya siku ya kupokea maombi.

iii. Pale ambapo mwanajumuiya/mwanachama anaomba uanachama atakubali kutii Kanuni za shirikisho,sheria na maadili ya kitanzania.

iv. Jumuiya itapaswa kulipa ada ya mwaka huo iliojiunga ndani ya siku 21 baada ya ombi la kujiunga kukubaliwa na Halmashauri Kuu.

## 10. Haki za Jumuiya

Kila Jumuiya mwanachama itakuwa na haki zifuatazo:-

i. Kushiriki katika shughuli zote za Shirikisho kwa utaratibu utakaowekwa.

ii. Kushiriki kwa uhuru kutoa maoni na mapendekezo katika mikutano na mikusanyiko ya Shirikisho kwa utaratibu utakaowekwa.

iii. Haki ya kuhudhuria na kutoa maoni kwenye mikutano ya Shirikisho.

iv. Haki ya kushiriki katika mikutano na shughuli zingine zinazohusika.

v. Kushirikishwa na kupewa taarifa katika mambo yanayogusa maslahi ya Shirikisho.

vi. Kupendekeza ajenda za vikao vya Shirikisho katika mikutano ya Shirikisho.

vii. Kupata nyaraka za Shirikisho kwa njia ya machapisho, vipeperushi, barua pepe, mitandao ya kijamii na njia nyengine yoyote kama hali itakavyoruhusu.

viii. Kuwakilisha Shirikisho katika mikutano itakayohitaji uwakilishi kama itakavyoamuliwana Uongozi.

ix. Kuwakilisha Shirikisho katika mikutano mbalimbali itakayohitaji uwakilishi wa Shirikisho kama itakavyoamuliwa na uongozi.

x. Haki ya kushiriki katika shughuli za Shirikisho kulingana na taratibu zilizowekwa

xi. Katika kufurahia haki hizi, Jumuiya mwanachama haitazitumia haki hizi kwa njia yoyote ambayo itaathiri haki za Jumuiya nyingine mwanachama.

xii. Jumuiya zote ni sawa ndani ya shirikisho bila kujali idadi ya wanachama au ukubwa wa jumuiya.

**11. Wajibu wa Jumuiya**

Kila Jumuiya mwanachama wa Shirikisho hili itakuwa na wajibu ufuatao:–

i. Kulinda, kuhifadhi, kutetea na kuitekeleza Kanuni hii wakati wote.

ii. Kulipa ada na michango mbalimbali ya Shirikisho kama itakavyoamuliwa na Shirikishokwa mujibu wa Kanuni hii.

iii. Kuwa mwaminifu na kutojihusisha na matumizi mabaya ya fedha au mali yoyote ya Shirikisho.

iv. Kufikisha taarifa mbalimbali za Shirikisho kwa wanachama wa Jumuiya husika kwa wakati husika.

v. Kuwahamasisha wanachama wa Jumuiya husika kushiriki shughuli mbalimbali za Shirikisho.

vi. Kutokujihusisha wala kushiriki masuala yahusuyo vyama vya siasa, au kuhusisha utendaji wa Shirikisho na mlengo wa chama fulani cha kisiasa.

**12. Ukomo wa Jumuiya**

Ukomo wa Jumuiya katika Shirikisho utazingatia mambo yafuatayo:-

i. Kufa kwa Jumuiya husika.

ii. Kuachishwa uanachama wa Shirikisho kwa uamuzi wa Mkutano Mkuu.

a. Shirikisho litasimamisha mwanachama yeyote au shirika ambalo limeweza kushiriki katika shughuli yoyote ambayo ni kinyume cha sheria au kinyume na masilahi ya Shirikisho.

b. Si chini ya siku 14 za kazi, barua ya kusimamishwa itatolewa, na itatolewa nafasi nzuri ya kujibu na kusikilizwa, au kutoa maoni kuhusu kusimamishwa kwa Jumuiya/Mwanachama.

c. Jumuiya/Mwanachama aliyesimamishwa atasimamishwa moja kwa moja kutekeleza

haki yoyote ya uanachama au marupurupu.

d. Mwanachama anaacha kuwa mwanachama siku 14 baada ya siku ambayo uamuzi wa kumsimamisha unawasilishwa kwake kwa maandishi.

iii. Jumuiya kujitoa yenyewe kwa maandishi baada ya kutoa sababu za msingi na maamuzi hayo kuridhiwa na kamati tendaji ya Shirikisho.

iv. Jumuiya kukosa uwakilishi katika vikao viwili vya Halmashauri Kuu ya Shirikisho mfululizo bila ya taarifa rasmi.

v. Jumuiya kukosa uwakilishi katika mikutano mikuu miwili mfululizo ya Shirikisho bila ya taarifa rasmi.

vi. Kutokulipa ada ya uanachama kwa awamu zote mfululizo bila ya taarifa rasmi.

vii. Kukiuka matakwa na masharti ya kanuni za Shirikisho.

viii. Viongozi wake kuingiza utendaji wa vyama vya siasa ndani ya Shirikisho/Jumuiya

ix. Kufa kwa Shirikisho.

**13. Jumuiya kujitoa katika Shirikisho**

i. Jumuiya mwanachama inaweza kujitoa kwenye Shirikisho kwa kuandika barua kuelezea nia yake hiyo kwa kamati tendaji na kamati tendaji itatafakari na kujadili ombi hilo na kutoa majibu ndani ya siku 28 za kazi.

ii. Iwapo ombi la Jumuiya kujitoa katika Shirikisho litakubaliwa, Jumuiya husika itatakiwa kufanya yafuatayo:-

a. Kulipa madeni yote inayodaiwa na Shirikisho.

b. Kurudisha mali zote za Shirikisho zilizokuwa katika Jumuiya husika.

c. Kufanya makabidhiano kwa maandishi.

## SEHEMU YA NNE: UONGOZI

**14. Uongozi wa Jumuiya Mwanachama**

i. Kila Jumuiya mwanachama itapaswa kuwa na viongozi watano pamoja na mwakilishi moja amabaye siyo kiongozi.

ii. Viongozwa Jumuiya watakuwa kama ifuatavyo:

(a) Mwenyekiti wa Jumuiya

(b) Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya

(c) Katibu Mkuu wa Jumuiya

(d) Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya

(e) Mweka hazina wa Jumuiya

(f)Mjumbe mmoja au mwakilishi wa Jumuiya katika mkutano mkuu wa TASAFIC

iii. Jumuiya zenye wanachama pungufu watakuwa na viongozi kulingana na idadi ya wanajumuiya wao.

iv. Jumuiya zeneye wanachama wasiofika sita (yaani wanachama 3-5) zitakuwa na viongozi kuanzia watatu.

v. Viongozi wa lazima kuwepo ili Jumuiya iweze kusajiliwa ni hawa wafuatao:

(a) Mwenyekiti wa Jumuiya

(b) Katibu Mkuu wa Jumuiya

(c) Mweka hazina wa Jumuiya

**15. Uongozi wa Shirikisho**
**A.**

i. Kiongozi wa Shirikisho ni kila Kiongozi toka kwenye Jumuiya Mwanachama mwenye dhamana yoyote katika Shirikisho aliyechaguliwa au kuteuliwa kwa mujibu wa Kanuni hii.

ii. Viongozi wa Jumuiya Wanachama watakuwa na haki ya kuchagua, kuchaguliwa au kuteuliwa kushika nafasi ya Uongozi wa Shirikisho hili kwa mujibu wa Kanuni hii

iii. Atakuwa na haki ya kutoa malalamiko kuhusu kukiukwa kwa malengo au madhumuni ya uanzishwaji wa Shirikisho mbele ya Halmashauri Kuu ya Shirikisho.

iv. Nafasi ya uongozi ndani ya jumuiya ndiyo itakuwa nafasi ya uongozi kwenye shirikisho.

**B**. Katika kuchagua viongozi wa Shirikisho, jumuiya itatekeleza yafuatayo:-

i. Kutoa Kiongozi katika nafasi moja kwa vipindi viwili mfululizo tu.

ii. Jumuiya iliyotoa Kiongozi wake katika nafasi moja kwa vipindi viwili mfululizo haitaruhusiwa kugombea nafasi hiyo mpaka baada ya kipindi kimoja kupita.

**16. Utaratibu wa upatikanaji wa viongozi**

i. Viongozi wa Shirikisho watapatikana kwa utaratibu ufuatao:

   a. Jumuiya inaweza kutoa Kiongozi katika nafasi moja kwa vipindi viwili mfululizotu.

   b. Jumuiya iliyotoa kiongozi wake katika nafasi moja kwa vipindi viwili mfululizo haitaruhusiwa kugombea nafasi hiyo mpaka baada ya kipindi kimoja kupita.

ii. Viongozi watachaguliwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu.

iii. Kila Jumuiya itakuwa na uwakilishi sawa katika uchaguzi ili kuleta uwiano na usawa (Isipokuwa kwa jumuiya ambazo zina viongozi wachache)

**iv. Tume ya uchaguzi.**

   a. Tume ya Uchaguzi itateuliwa na Mwenyekiti wa Kamati Tendaji na kupitishwa na Halmashauri Kuu kwa kura za ndio au hapana.

   b. Endapo kura za hapana zitakuwa nyingi Mwenyekiti wa Shirikisho atatakiwa kushughulikia maoni ya halmashauri kuu baada ya kuikataa Tume ya Uchaguzi.

   c. Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi wanapaswa kuwa viongozi na wanajumuiya.

   d. Tume ya Uchaguzi itaongozwa na Mwenyekiti wa Tume, Katibu wa Tume, na wajumbe watatu.

   e. Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi anatakiwa kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ambaye muda wake unaisha na hajagombea nafasi yoyote.

   f. Katibu wa Tume anapaswa kuwa Mjumbe wa Sekretarieti ya Shirikisho.

g. Wajumbe wa Tume wanaweza kutoka ndani ya wajumbe wa Mkutano Mkuu.

h. Wawakilishi wa wagombea watateuliwa na wagombea husika na jukumu lao litakuwa kuhakiki utaratibu wa kuhesabu kura na kutangaza matokeo tu.

i. Wawakilishi wa wagombea wataripoti kwa Mwenyekiti wa Kamati Tendaji endapokuna malalamiko yeyote juu ya tume.

j. Mwenyekiti wa Kamati Tendaji atakapojiridhisha na malalamiko ya wawakilishi atakuwa na nafasi ya kutengua uongozi wa tume au tume yote na kubatilisha utendaji wote wenye makosa.

k. Baada ya kubatilisha utendaji wa Tume, Mwenyekiti atateua Tume mpya ya Uchaguzi na kupitishwa ndani ya siku 14 za kazi na zoezi la Uchaguzi kuanza upya.

l. Muda wa kampeni, uchaguzi na matokeo utaratibiwa na Tume ya Uchaguzi.

m. Tume ya Uchaguzi itakuwa huru na itafuata kanuni za Katiba hii sambamba na kutunza vizuri nyaraka na kufanya uhakiki wa wapiga kura.

**v. Wagombea**

a. Wagombea watachukua fomu kujaza na kurejesha kwa mujibu wa kanuni namba 26.

b. Watafanyiwa usaili na Tume ya Uchaguzi na matokeo kutangazwa punde baadaya usaili kuisha.

c. Wagombea ambao hawakupita kwenye usaili watakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Tume kwa mara ya kwanza na kwa mara ya pili kwa kamati tendaji. Kushindwa kwa rufani zote kunaashiria kushindwa kupita kwenye usaili.

d. Tume ya Uchaguzi itahakikisha kuna wagombea zaidi ya mmoja kwa kila nafasi ya labda pale itakapolazimu na tume italazimika kutoa sababu za kutokea hilo kwa wajumbe wa Mkutano Mkuu.

e. Tume ya Uchaguzi itatakiwa kuratibu zoezi la kampeni kwa njia ya mtandao na ana kwa ana, na kuweka masharti ya kampeni kwa mujibu wa muktadha husika wa

uchaguzi.

f. Mgombea atapaswa kufanya kampeni kwa muda wake aliopangiwa tu

g. Mgombea atakaekiuka muda wa kampeni atafutwa kwenye idadi ya wagombea na atakuwa amekosa sifa ya kushiriki uchaguzi

h. Kampeni zitakazoendeshwa kwa njia ya siri hazitaruhusuiwa kufanyika.

i. Kipindi chote cha uchaguzi, mgombea wala wapambe wa mgombea hawatapaswa kuwafuata wajumbe/wapiga kura kwa siri na kuwashawishi kwa namna tofauti na maelekezo ya kampeni.

j. Mawasiliano ya siri nje ya utaratibu uliowekwa yatatafsirika kama rushwa kipindi cha uchaguzi na mgombea/wapambe wa mgombea watakao bainika wataenguliwa majina yao.

k. Mgombea atakaetoa rushwa atafutwa kushiriki uchaguzi na atakuwa chini ya uangalizi wa Halmashauri Kuu kujibu mashtaka yake na hatua za kinidhamu kuchukuliwa dhidi yake au wapambe wake.

l. Ili kuweka mazingira sawa ya kampeni, viongozi wa Jumuiya anayotokea mgombea hawataruhusiwa kushiriki kampeni kwa namna yeyote ile, wazi au kwasiri.

m. Tume itasimamia zoezi la kupiga kura kwa kushirikiana na wawakilishi wa wagombea mpaka pale Tume itakapotangaza matokeo.

n. Wapiga kura watakuwa viongozi wote wa Jumuiya zote hai yaani Jumuiya zilizolipa ada zao za uanachama, ambao wanashika nyadhifa sita kutoka kila jumuiya

   i. Mwenyekiti na Makamu wake
   ii. Katibu na Makamu wake
   iii. Mhazini na Mwakilishi wa Mkutano Mkuu wa TASAFIC (ambaye huteuliwa na jumuiya)

o. Namna ya kupiga kura itaratibiwa na Tume ya Uchaguzi kulingana na muktadha wa uchaguzi (aidha kwa njia ya mtandao au ana kwa ana).

p. Kiongozi atakaebainika kutumia udanganyifu katika upigaji wa kura atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwemo karipio la maandishi au kuvuliwa nyadhifa yake.

q. Mgombea atakaebainika kutumia udanganyifu ataondolewa kwenye kinyang'anyiro na matokeo yake yote yatakuwa batili.

r. Malalamiko ya uchaguzi baada ya matokeo yatawasilishwa kwa mamlaka ya uteuzi wa Tume ya Uchaguzi ndani ya masaa matatu (3).

**ii. Matokeo**

a. Matokeo yatatangazwa na pingamizi litakaribishwa ndani ya masaa matatu

b. Iwapo hakuna pingamizi, Mwenyekiti wa Tume atakabidhi majina ya washindi aliowatangaza kwa Mwenyekiti wa Kamati Tendaji na ripoti ya uchaguzi mzima

**iii. Kuapishwa**

a. Viongozi waliochaguliwa watakula kiapo mbele ya Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi

b. Viongozi watakabidhiwa ofisi mara baada ya Mwenyekiti anaemaliza muda wake kuivunja Tume ya Uchaguzi

**17. Sifa za kiongozi**

Pamoja na kutimiza masharti ya Uanachama kama yalivyoelezwa katika Kanuni hizi, mtu atafaa kuwa kiongozi kwa kuwa na sifa zifuatazo:-

i. Awe Kiongozi kutoka katika Jumuiya mwanachama.
ii. Awe muadilifu, mkweli na mwaminifu.
iii. Awe anayekubali kujisahihisha, kusahihishwa na akubali kuwajibika
iv. Asiwe na rekodi ya tabia mbaya za kinidhamu na zisizo za kimaadili.
v. Asiwe na rekodi ya makosa ya jinai.
vi. Awe na rekodi ya kuhudhuria vikao na shughuli mbalimbali za Shirikisho.
vii. Aoneshe utayari wa kujitolea kuongoza Shirikisho.
viii. Jumuiya yake iwe imekamilisha michango na madeni yote ndani ya Shirikisho.
ix. Awe na uelewa mkubwa wa masuala ya Shirikisho, kanuni na taratibu zake.
x. Yote haya yatafuatwa kwa kuzingatia kanuni namba 26 yote.

## 18. Miiko ya Kiongozi

Ni mwiko kwa kiongozi wa Shirikisho kufanya yafuatayo:-

i. Kutumia madaraka aliyopewa kwa ajili ya manufaa yake binafsi, au kwa upendeleo au kwa namna yoyote ambayo ni kinyume cha lengo lililokusudiwa madaraka hayo.

ii. Kutoa maelezo, taarifa au siri za Shirikisho kwa mtu au chombo chochote bila ya idhini ya mamlaka inayohusika.

iii. Kupokea mapato ya kificho, kutoa au kupokea rushwa au kushiriki katika mambo yoyote ya magendo.

iv. Kutumia nafasi yake ya uongozi kuwa wakala au kuhamasisha itikadi za vyama vya siasa katika shirikisho.

v. Kuwabagua wanajumuiya kwa itikadi za vyama vya siasa

vi. Kuonesha upendeleo wa wazi kwa Jumuiya yake tu na sio kwa Shirikisho kwa ujumla

vii. Kujihusisha na masuala ya vyama vya kisiasa awapo madarakani.

## 19. Ukomo wa uongozi

Kiongozi atafikia ukomo wa uongozi wake kutokana na yafuatayo:-

i. Jumuiya yake Kukoma Uanachama kwenye Shirikisho.
ii. Muda wake wa uongozi kumalizika.
iii. Kuhitimu masomo yake.
iv. Kujiuzulu mwenyewe kwa kuandika barua kwa Kamati Tendaji.
v. Kufariki dunia.
vi. Kupata dharura binafsi itakayopelekea kutokuwepo katika Jamhuri ya watu wa China kwa muda wa miezi sita mfululizo isipokuwa tu itakapothibitishwa vinginevyo na Halmashauri Kuu na Kamati Tendaji.
vii. Kuondolewa kutokana na kukiuka kwa makusudi Kanuni za Shirikisho.
viii. Kupata ugonjwa utakaoathiri utendaji wake wa kazi na kuthibitishwa na madaktari.
ix. Theluthi mbili ya Jumuiya wanachama kutokuwa na imani naye.

x. Kiongozi aliyeachishwa, kufukuzwa au kuondolewa uongozi hatakuwa na haki ya kuomba tena uongozi kwa awamu mbili hadi tatu za uongozi.

**20. Viongozi wakuu wa Shirikisho**

Kutakuwa na Viongozi Wakuu wa Shirikisho wafuatao:–

i. Mwenyekiti wa Shirikisho.

ii. Makamu Mwenyekiti wa Shirikisho.

iii. Katibu Mkuu wa Shirikisho.

iv. Naibu Katibu Mkuu wa Shirikisho.

v. Mweka hazina wa Shirikisho.

**21. Mwenyekiti wa Shirikisho**

Mwenyekiti kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi:-

i. Atakuwa ndiye msemaji mkuu na mwakilishi wa Shirikisho katika ubalozi na shughuli nyingine za nje kwa niaba ya Shirikisho.
ii. Ndiye msimamizi mkuu wa shughuli zote za Shirikisho.

iii. Kwa kushauriana na Kamati tendaji ana mamlaka ya kumteua Kiongozi toka kwenye Jumuiya mwanachama yoyote kuwakilisha Shirikisho katika shughuli za nje ya Shirikisho.

iv. Atakuwa ndiye Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu, Halmashauri Kuu na Kamati Tendaji ya Shirikisho.

v. Atakuwa na mamlaka ya uteuzi wa Kamati mbalimbali za Shirikisho.

vi. Atakuwa na mamlaka ya uteuzi wa Tume ya Uchaguzi wa Shirikisho na kutengua.

vii. Kiongozi wa halmashauri kuu pamoja na Mkutano mkuu.

viii. Zaidi ya kuwa na kura yake ya kawaida katika Mikutano anayoingoza, atakuwa pia na kura ya uamuzi endapo kura za wajumbe wanaoafiki na wasioafiki zitalingana.

ix. Kutoa taarifa za msiba ikitokea mwanashirikisho/mwanajumuiya amefariki.

x. Atashirikiana na Makamu Mwenyekiti kwa kila jambo linalohusu Shirikisho.

**22. Makamu Mwenyekiti wa Shirikisho**

Makamu Mwenyekiti kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi:-

i. Atakuwa ndiye msaidizi mkuu wa Mwenyekiti wa Shirikisho na atafanya kazi zote za Shirikisho atakazopewa na Mwenyekiti wa Shirikisho.

ii. Atashauriana na Mwenyekiti wa Shirikisho katika kila hatua ya uendeshaji wa shughulizote za Shirikisho.

**23. Katibu Mkuu wa Shirikisho**

Kwa kuzingatia masharti ya kanuni hizi:-

i. Atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa Shirikisho na atafanya kazi chini ya Uongozi waKamati Tendaji.

ii. Atakuwa ndiye mratibu wa shughuli zote za Shirikisho.

iii. Atatunza kumbukumbu na nyaraka zote za Shirikisho.

iv. Atakuwa ndiye Katibu wa Mkutano Mkuu, Halmashauri Kuu na Kamati Tendaji na ataandika muhtasari wa kikao husika.

v. Atakuwa ndiye Mwenyekiti wa Sekretarieti ya Shirikisho.

vi. Atafanya kazi nyingine za Shirikisho kama atakavyoelekezwa na Mwenyekiti.

vii. Atasaidiana na Naibu Katibu Mkuu katika kutekeleza majukumu ya shughuli zake.

**24. Naibu Katibu Mkuu wa Shirikisho**

Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi:-

i. Atakuwa ndiye msaidizi mkuu wa Katibu Mkuu, na katika wadhifa wake huo,atawajibika kwa Katibu Mkuu katika utendaji wa kila siku.

ii. Atashauriana na Katibu Mkuu katika uratibu na utendaji wa shughuli zake.

iii. Atakuwa ndiye Katibu wa vikao vya Sekretarieti.

**25. Mweka Hazina wa Shirikisho**

Mweka Hazina wa Shirikisho:-

i. Atakuwa ndiye msimamizi wa masuala yote ya uchumi na fedha wa Shirikisho.

ii. Atatoa taarifa zihusuzo mapato na matumizi ya Shirikisho katika vikao vyote vya Shirikisho na kila miezi mitatu kwa wanashirikisho kupitia Wahazini wa Jumuiya zote.

iii. Atatunza taarifa zote za fedha na bidhaa za Shirikisho na kuhakikisha makabidhiano yanaenda vizuri baina yake na Mweka Hazina atakayempokea.

iv. Atashirikiana na Kamati Tendaji na Mlezi katika kutafuta na kusimamia vyanzo vya mapato ya Shirikisho.

v. Atafuatilia Jumuiya wanachama kulipa ada na michango mbalimbali ya Shirikisho.

vi. Atabuni njia mbalimbali halali za kuongeza mapato ya Shirikisho.

vii. Atakuwa ndiye Mwenyekiti wa Kurugenzi ya Uchumi na Fedha.

**26. Njia za Upatikanaji wa Viongozi wa Shirikisho**

Viongozi watapatikana kwa kufuatwa njia zifuatazo:-

i. Kujaza fomu maalum zenye kuelezea wasifu wa mhusika.
ii. Nafasi ya Mwenyekiti wa Shirikisho itaombwa na Mwenyekiti au Rais wa Jumuiya mwanachama.
iii. Nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Shirikisho itaombwa na Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya mwanachama.
iv. Nafasi ya Katibu Mkuu wa Shirikisho itaombwa na Makatibu Wakuu wa Jumuiya wanachama.
v. Nafasi ya Naibu Katibu wa Shirikisho itaombwa na Naibu Makatibu wa Jumuiya wanachama.
vi. Nafasi ya Mweka Hazina itaombwa na Waweka Hazina wa Jumuiya wanachama.
vii. Viongozi watachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Jumuiya wanachama na watadumu madarakani kwa muda wa mwaka mmoja.
viii. Viongozi wataelezea sera zao na mipango yao kwa Shirikisho katika Mkutano Mkuu kabla ya kufanya uchaguzi.
ix. Kiongozi atapatikana kwa kupigiwa kura na wajumbe kwenye mkutano mkuu na kutangazwa mshindi kwa kupata kura nyingi zaidi ya mgombea au wagombea wenzake.
x. Ikitokea nafasi wazi kwenye Uongozi, nafasi hiyo itajazwa kwa kufanyika uchaguzi mdogo wa dharura ili kuiziba nafasi hiyo.
xi. Iwapo italazimu kuwa na mgombea mmoja katika nafasi yoyote, mgombea husika atapigiwa kura za NDIYO au HAPANA.
xii. Uchaguzi Mkuu utafanyika kati ya mwezi wa sita (6) kila mwaka.
xiii. Wakati wa Uchaguzi Mkuu, Kamati Tendaji itaweka utaratibu unaofaa katika kufanikisha uchaguzi huo.

**27. Mlezi wa Shirikisho**

i. Balozi wa Tanzania katika Jamhuri ya watu wa China atakuwa ndiye mlezi waShirikisho.

ii. Ili kuleta mshikamano baina ya Shirikisho na ubalozi, mlezi wa Shirikisho atakuwa na majukumu yafuatayo:-

a. Kuwa Mshauri Mkuu wa shughuli za Shirikisho;

b. Kutoa mapendekezo kwa uongozi wakati wowote itakapohitajika kwa mujibu wa Kanuni hizi.

## SEHEMU YA TANO: VIKAO, KURUGENZI NA KAMATI ZA SHIRIKISHO

### 28. Vikao vya Shirikisho

Kutakuwa na Vikao vya Shirikisho vifuatavyo:–

iii. Mkutano Mkuu wa Shirikisho.

iv. Halmashauri Kuu ya Shirikisho.

v. Kamati Tendaji ya Shirikisho.

vi. Sekretarieti ya Shirikisho.

vii. Kurugenzi ya Uchumi na Fedha

viii. Kamati za TASAFIC

### 29. Mkutano Mkuu wa Shirikisho

Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Shirikisho utakaokuwa na wajumbe wafuatao:-

i. Mwenyekiti wa Shirikisho.

ii. Makamu Mwenyekiti wa Shirikisho.

iii. Katibu Mkuu wa Shirikisho.

iv. Naibu Katibu Mkuu wa Shirikisho.

v. Mweka Hazina wa Shirikisho.

vi. Mwenyekiti wa kila Jumuiya mwanachama.

vii. Makamu Mwenyekiti au Makamu wa kila Jumuiya mwanachama.

viii. Katibu Mkuu wa kila Jumuiya mwanachama.

ix. Naibu Katibu Mkuu wa kila Jumuiya mwanachama.

x. Mweka Hazina wa kila Jumuiya Mwanachama.

xi. Kutakuwa na mjumbe mmoja kutoka kila Jumuiya mwanachama ambaye sikiongozi. Jumuiya husika itaandaa utaratibu wa kumpata mjumbe huyo.

xii. Mgeni Rasmi atakayependekezwa na Kamati Tendaji.

xiii. Wageni waalikwa watakaohudhuria kutizama bila kuwa na ujumbe hawatakuwa na nafasi ya kuchangia hoja (Wageni waalikwa wanaweza kuwa wajumbe wa kamati mbalimbalimbali, wanajumuiya wote na waliowahi kuwa wanajumuiya na wakapenda kushiriki).

**30. Kazi na uwezo wa Mkutano Mkuu**

Mkutano Mkuu ndicho kikao kikuu kupita vikao vyote vya Shirikisho na utakuwa kazi na uwezokama ifuatavyo:-

i. Kupokea na kujadili taarifa ya kazi za Shirikisho zilizotolewa na Halmashauri Kuu na kutoa maelekezo ya mipango na utekelezaji wa malengo kwa kipindi kijacho.

ii. Kuthibitisha, kubadili au kutengua mapendekezo yaliyotolewa na kikao chochote chachini yake au na kiongozi wa Shirikisho.

iii. Kumuadhibu, kumwachisha au kumfukuza uongozi, kiongozi yeyote wa Shirikisho ambaye atathibitika kwenda kinyume na Kanuni hizi.

iv. Kupokea na kusikiliza utetezi na rufaa zilizowasilishwa na mwanachama au kiongozidhidi ya tuhuma zinazomkabili au adhabu aliyopewa na vikao vya chini yake.

v. Kupokea taarifa zote za mapato na matumizi ikiwa ni pamoja na mipango mikakati kwa mwaka mzima.

vi. Kubadili sehemu yote ya Kanuni za Shirikisho kwa uamuzi wa theluthi mbili za wajumbe.

vii. Kupitisha Kamati ndogo za Shirikisho zilizoteuliwa na Mwenyekiti kwa kadri itakavyoonekana inafaa ili kutekeleza shughuli za Shirikisho.

viii. Kuchagua na kupitisha viongozi wakuu wa Shirikisho wakati wa uchaguzi.

**31. Vikao vya Mkutano Mkuu**

i. Mkutano Mkuu kwa kawaida utakutana kila miezi mitatu yaani jumla ya vikao vinne kwa mwaka lakini unaweza kukutana kwa dharura wakati mwengine wowote pale itakapohitajika (Taarifa za uwepo wa Mkutano huu zitatolewe wiki mmoja kabla).

ii. Maazimio madogo ya dharura yanaweza kupitishwa ndani ya kundi sogozi la mkutano mkuu kwa kutolewa tangazo/notisi ya siku tatu.

iii. Mwenyekiti wa Shirikisho atakuwandiye Mwenyekiti wa vikao vya mkutano mkuu.

iv. Mwenyekiti asipokuwepo Makamu wake ataendesha kikao.

v. Endapo wote wawili hawapo, mkutano utachagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wa kikao hicho.

**32. Akidi ya vikao vya Mkutano Mkuu**

i. Akidi ya Mkutano Mkuu wa Shirikisho itakuwa ni theluthi mbili ya wajumbe wa Jumuiya wanachama.

ii. Akidi pungufu itahesabika kwa Jumuiya hai kwa kipindi hicho endapo ushiriki wa Jumuiya nyingine utakuwa ni wa kusita na Kamati Tendaji itaandika barua ya onyo kwa Viongozi wasioshiriki Mkutano huu.

**33. Maamuzi ya vikao**

i. Maamuzi ya vikao yatafanywa kwa makubaliano.

ii. Iwapo makubaliano hayakufikiwa, maamuzi yatafanyika kwa kupigiwa kura.

iii. Endapo kura zitakuwa sawa, Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Shirikisho au mjumbe anayeendesha kikao atakuwa na kura ya maamuzi.

## 34. Halmashauri kuu ya Shirikisho

Halmashauri kuu ya Shirikisho itakuwa na wajumbe wafuatao:–

i. Mwenyekiti wa Shirikisho.
ii. Makamu Mwenyekiti wa Shirikisho.
iii. Katibu Mkuu wa Shirikisho.
iv. Naibu Katibu Mkuu wa Shirikisho.
v. Mweka Hazina wa Shirikisho.
vi. Mwenyekiti au Rais wa kila Jumuiya mwanachama.
vii. Makamu Mwenyekiti wa kila Jumuiya mwanachama.

## 35. Kazi na uwezo wa Halmashauri Kuu

Halmashauri Kuu ya Shirikisho itakuwa na kazi na uwezo kama ifuatavyo:-

i. Kuandaa Mkutano Mkuu wa Shirikisho.

ii. Kupokea na kujadili taarifa ya kazi za Kamati Tendaji ya Shirikisho.

iii. Kuleta mapendekezo ya kujiunga au kujitoa kwenye umoja au uhusiano na taasisi mbalimbali kwa kulinda maslahi ya Shirikisho.

iv. Kupendekeza marekebisho ya muundo wa Shirikisho katika maeneo na nyanja mbalimbali kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

v. Kupendekeza kwa mkutano mkuu kusimamisha uanachama wa Jumuiya yoyote au kumvua madaraka Kiongozi wa shirikisho endapo itathibitika kuwa mwenendo wake unakiuka matakwa ya Kanuni hizi.

vi. Kubadili kifungu chochote cha Kanuni na kufanya maamuzi yanayohusu uendeshaji wa Shirikisho kwa kadri itakavyoonekana inafaa kwa niaba ya Mkutano Mkuu wa Shirikisho na kuwasilisha mapendekezo hayo kwa Mkutano Mkuu.

vii. Kumchukulia hatua za kinidhamu kiongozi au mjumbe yeyote atakayekiuka matakwa ya Kanuni hizi ikiwemo karipio la mdomo, maandishi, kusimamishwa uongozi au kuzuiwa

kujishughulisha na shughuli zozote za Shirikisho ama hatua nyengine yoyote kama itakavyoonekana inafaa.

viii. Kupitisha makisio ya mapato na matumizi ya Shirikisho.

ix. Kuandaa mipango na mikakati ya utendaji kwa kila mwaka ikiwa ni pamoja na kubuni njia mbalimbali za kukuza Shirikisho na kufanya kuwa kiungo miongoni mwa wanafunzi wanaosoma nchini China.

x. Kupitisha wateule waTume ya uchaguzi kwa kura ya ndio au hapana.

xi. Endapo watasema hapana wajumbe wengi watatoa sababu na mapendekezo ya majina.

**36. Vikao vya Halmashauri Kuu**

i. Halmashauri Kuu itafanya mikutano yake ya kawaida mara nne kwa mwaka yaani kabla ya Mkutano Mkuu isipokuwa tu pale itakapohitajika vinginevyo, inaweza kufanya mikutano ya dharura wakati wowote.

ii. Mkutano wa kwanza utakuwa ndani ya robo ya kwanza kwa ajili ya kujadili na kupitisha kamati mbambali za TASFIC.

iii. Mkutano wa pili na wa tatu itapangwa ndani ya robo ya pili na ya tatu kwa kadri kamati tendaji itakavyoona inafaa (Maandaizi ya mkutano mkuu wa tatu na wa nne).

iv. Mkutano wa nne utakuwa ndani ya robo ya nne yaani mwezi Juni na utakuwa kwa ajili ya maandalizi ya uchaguzi na kuhitimisha safu ya uongozi.

v. Mwenyekiti wa Shirikisho atakuwa ndiye Mwenyekiti wa Mkutano wa halmashaui kuu na asipokuwepo Makamu wake ataendesha mkutano. Endapo wote wawili hawapo, mkutano utachagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wa mkutanohuo.

**37. Kamati Tendaji ya Shirikisho**

Kamati Tendaji ya Shirikisho itakuwa na wajumbe wafuatao:-

i. Mwenyekiti wa Shirikisho.

ii. Makamu Mwenyekiti wa Shirikisho.

iii. Katibu Mkuu wa Shirikisho.

iv. Naibu Katibu Mkuu wa Shirikisho.

v. Mweka hazina wa Shirikisho.

**38. Kazi za Kamati Tendaji**

Kamati tendaji itakuwa na kazi zifuatazo:-

i. Kuandaa mikutano ya Halmashauri Kuu ya Shirikisho.

ii. Kuratibu na kutekeleza majukumu ya kila siku ya Shirikisho na kuhakikisha malengo na madhumuni ya Shirikisho yaliyowekwa yanafikiwa.

iii. Kupokea taarifa za kazi za Sekretarieti, Kurugenzi ya Uchumi na Fedha na Kamati za Shirikisho.

iv. Kushughulikia uhusiano kati ya Shirikisho na Jumuiya au Taasisi mbalimbali zilizopo ndani na nje ya China zinazohusiana na Shirikisho.

v. Kutoa mapendekezo ya kujiunga au kujitoa kwenye umoja au uhusiano na taasisi mbalimbali kwa kulinda maslahi ya Shirikisho.

vi. Kupendekeza marekebisho ya Muundo wa Shirikisho katika maeneo na nyanja mbalimbali na kuyapeleka kwenye Halmashauri Kuu kwa ajili ya utekelezaji kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

vii. Kuwa ni daraja kati ya Ubalozi na Jumuiya za wanafunzi juu ya mambo yote yahusuyo Wanafunzi waliopo katika Jamhuri ya watu wa China.

viii. Kupokea na kushughulikia masuala yote yanayohusu wanafunzi yatakayowasilishwa na Jumuiya wanachama nakuyafikisha sehemu husika.

ix. Kuratibu mikutano midogo midogo ya makundi sogozi ya tafiti na kundi la wanawake.

**39. Vikao vya kamati tendaji**

i. Kamati Tendaji itafanya mikutano yake ya kawaida mara moja kwa mwezi isipokuwa tu pale itakapohitajika vyenginevyo, inaweza kufanya mikutano ya dharura wakati wowote.

ii. Mwenyekiti wa Shirikisho atakuwa ndiye Mwenyekiti wa Mkutano wa Kamati Tendaji na asipokuwepo Makamu wake ataendesha mkutano. Endapo wote wawili hawapo, mkutano utachagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wa mkutanohuo.

iii. Pale patakapokuwa na mikutano elimishi kutoka kundi la wanawake wa TASAFIC au kundi la tafiti, kwa kila siku ya Jumamosi.

**40. Sekretarieti ya Shirikisho**

Sekretarieti ya Shirikisho itakuwa na wajumbe wafuatao;

i. Katibu mkuu wa Shirikisho.

ii. Naibu Katibu Mkuu wa Shirikisho.

iii. Makatibu wa kila Jumuiya mwanachama wa Shirikisho.

iv. Manaibu Katibu wa kila Jumuiya mwanachama wa Shirikisho

**41. Kazi za Sekretariet ya Shirikisho**

Sekretarieti ya Shirikisho itakuwa na kazi zifuatazo:-

i. Kutekeleza shughuli za kila siku za shirikisho na maazimio ya vikao vya Shirikisho.

ii. Kuandaa shughuli za vikao vya Shirikisho.

iii. Kuandaa na kusimamia utaratibu wa mapokezi ya wanafunzi wapya wanaowasili kwamara ya kwanza katika Jamhuri ya watu wa China.

iv. Kufuatilia mambo yote yanayohusu udhamini na mikopo ya wanafunzi wanufaika waBodi ya mikopo ya Elimu ya Juu na taasisi nyengine za udhamini.

v. Kufuatilia fursa mbalimbali za ufadhili wa masomo katika Jamhuri ya watu wa Chinana kuzitangaza kwa Watanzania.

vi. Kutoa taarifa za kielimu na zote zihusuzo wanafunzi kwenye njia za mawasiliano za Shirikisho.

vii. Kuratibu midahalo mbalimbali ya kielimu kwa wanachama wake.

viii. Kufuatilia ubora wa hali ya elimu na maisha ya wanafunzi watanzania kwenye vyuo mbalimbali katika Jamhuri ya watu wa China na kutoa mapendekezo kwa Wizara ya elimu ya Tanzania kupitia Ubalozi.

ix. Kuwasilisha taarifa yake ya kazi na kuwajibika kwa Kamati Tendaji ya Shirikisho.

x. Kutoa mapendekezo ya kitaalamu kwa Vikao vya juu ya namna ya kutumia fursa zilizopo katika Jamhuri ya watu wa China kwa maslahi ya Tanzania ili mapendekezo hayo yaweze kuwasilishwa Ubalozini na kwenye mamlaka husika nchini Tanzania.

xi. Kuwa chimbuko la kuibua na kukusanya mawazo na taarifa mbalimbali kutoka kwa wanafunzi na wadau wa Shirikisho.

xii. Kusimamia makundi sogozi yote ya mitandao ya WhatsApp na Wechat, kusimamia mitandao ya kijamii ya Shirikisho

**42. Vikao vya Sekretarieti**

xiii. Sekretarieti kwa kawaida itakutana mara moja kwa mwezi kati ya mwezi lakini inaweza kukutana kwa dharura wakati mwengine wowote pale itakapohitajika.

xiv. Katibu Mkuu atakuwa ndie Mwenyekiti wa Mkutano wa Sekretarieti na asipokuwepo Naibu wake ataendesha mkutano. Endapo wote wawili hawapo, mkutano utachagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wa mkutano huo.

**43. Kurugenzi na Kamati za Shirikisho**

Kutakuwa na kurugenzi na kamati za Shirikisho kama ifuatavyo:-

**44. Kurugenzi ya Uchumi na Fedha**

Kurugenzi ya Uchumi na Fedha itakuwa na wajumbe wafuatao:-

i. Mweka Hazina wa Shirikisho.

ii. Mweka Hazina wa kila Jumuiya mwanachama.

iii. Mjumbe mmoja kutoka kila Jumuiya mwanachama (Mwakilishi wa TASAFIC).

**45. Kazi za Kurugenzi**

Kazi za Kurugenzi ya Uchumi na Fedha zitakuwa:-

i. Kukusanya ada na michango kutoka kwa jumuiya wanachama.

ii. Kubuni miradi mbalimbali kwa ajili ya kuongeza pato la Shirikisho.

iii. Kudhibiti matumizi ya pesa za Shirikisho na kuhakikisha zinatumika kadiri ya Kanuni za Shirikisho au matumizi yaliyoamuliwa na vikao halali vya Shirikisho.

iv. Kutunza mahesabu ya Shirikisho kwa ajili ya kumbukumbu katika vikao mbalimbali vya Shirikisho.

v. Kushauri namna bora ya Utunzaji wa fedha za Shirikisho.

vi. Kusimamia na kuidhinisha matumizi ya fedha za Shirikisho.

vii. Kuwasilisha taarifa yake ya kazi kwa Kamati Tendaji.

viii. Kurugenzi itakuwa na vikao kulingana na uhitaji walau kila miezi mitatu kabla ya Mkutano Mkuu na wakati mwingine wowote kadiri itakavyohitajika.

ix. Mweka Hazina wa Shirikisho ndiye ataongoza kurugenzi hii.

x. Mjumbe mwenye utaalamu wa Uchumi na Fedha atateuliwa na Kamati Tendaji kwa kufuata kigezo cha umahiri wake katika fani ya Uchumi na fedha.

**46. Kamati za Shirikisho**

Kutakua na kamati maalumu zifuatazo:-

a. Kamati ya Elimu na fursa za masomo (HEoCT).

b. Kamati ya fursa za biashara.

c. Kamati ya tuzo.

d. Kamati ya michezo, Hamasa na Uhusiano.

e. Kamati nyingine kwa kadri Mwenyekiti wa kamati tendaji atakavyoona inafaa.

i. Kamati hizi zitateuliwa na Kamati Tendaji na kupitishwa na mkutano mkuu baada ya uteuzi ndani ya kundi sogozi la mkutano mkuu kwa kura za ndio au hapana, kwa notisi ya siku tatu

ii. Kamati zitapangiwa majukumu ya jumla na Mwenyekiti wa Kamati Tendaji na kupewa uhuru wa kuweka nyongeza ya kiutendaji.

iii. Mwenyekiti anaweza kuteua kamati nyingine tofauti na zilizoainishwa kulingana na uhitaji wa wakati huo

iv. Mwenyekiti wa kamati tendaji anabaki na haki ya kutengua uteuzi wa mjumbe wakati wowote

ule atakapo fanya majukumu yake vibaya au atakapo koma kushiriki majukumu yake kikamilifu

v. Kamati hizi zitakutana kulingana na majukumu yao ya kiutendaji na zitapewa vyeti/tunzo kulingana na utendaji wao.

## SEHEMU YA SITA: MFUKO WA SHIRIKISHO

### 47. Mfuko wa Shirikisho na Utaratibu wa Matumizi.

i. Mfuko ulianzishwa kwa lengo la kumkopesha mwanajumuiya anayepatwa na tatizo la ugonjwa kwa ajili ya matibabu pale inapohitajika.

ii. Kila Jumuiya itawasilisha kwa Shirikisho mchango wa mfuko wa kama itakavyoainishwa na halmashauri kuu kulingana na wakati husika, mahitaji na hali ya Jumuiya.

iii. Fedha ya ada ya kila mwaka itaingia moja kwa moja kwenye mfuko na matumizi ya Shirikisho yatakayopitishwa yatatokea kwenye mfuko huu.

iv. Matumizi ya mfuko huu ni yafuatayo:-

a. Rambirabi kwa mwanajumuiya anayetokea Jumuiya mwanachama hai.
b. Safari za kiofisi za Viongozi wakuu wa TASAFIC.
c. Miradi ya kutunisha mfuko wa TASAFIC.
d. Malipo ya tovuti ya Shirikisho.
e. Kuratibu Mkutano Mkuu
f. Matumizi mengineyo kwa ajili ya Shirikisho ambayo hayajaorodheshwa yatawasilishwa kwa Mweka Hazina wa Shirikisho na kujadiliwa na Kurugenzi hii kisha kupitishwa au kutopitishwa kwa kupigiwa kura.

v. Kama mfuko hautajitosheleza, mchango utaombwa kwa wanajumuiya na pesa zitakazopatikana zitaingia kwenye mfuko.

vi. Muhitaji atakopeshwa kwa maandishi na wadhamini wawili, amana ya pasi ya kusafiria itaifadhiwa na Mhazini wa Jumuiya yake mpaka pale mdaiwa atakaporejesha pesa alizokopeshwa.

vii. Nakala ya fomu ya kuomba mkopo na barua ya maombi zitahifadhiwa na Mweka hazina.

viii. Muhitaji atawasilisha kila kitakachohitajika kuthibitisha uhitaji wake kwa ajiliya ukaguzi.

viii. Baada ya pesa kutolewa zitawekwa chini ya usimamizi wa Mweka hazina wa shirikisho ambapo atafanya malipo kwa mhitaji.

ix. Pasi ya kusafiria haitarejeshwa mpaka deni litakapolipwa.

x. Deni litadumu ndani ya miezi mitatu tu baada ya kukopeshwa.

xi. Muda wa marejesho ni miezi mitatu toka amekopeshwa

xii. Mwanachama atakayekopeshwa ni yule ambaye yupo kwenye kanzidata ya Shirikisho kutoka kwa Katibu wa Jumuiya yake, kama jina halitakuwepo mwanachama yule atapoteza vigezo vya kukopeshwa.

xiii. Mfuko ni kwa dharura za kiafya zinazo wahusu wanachama hai tu, dharura zingine zinaweza kuridhiwa na Halmashauri Kuu ili muombaji akopeshwe.

xiv. Mikopo yote itawasilishwa kwa Katibu Mkuu na itajadiliwa na Kamati Tendaji na hatimaye kuwasilishwa kwa Halmashauri Kuu kwa ajili ya kupitishwa kwa kura ya ndio au hapana.

xv. Mikopo yote haitakuwa na riba.

xvi. Endapo mwanajumuiya aliyekopeshwa fedha za mfuko atafariki kabla ya kurejesha fedha hizo, Shirikisho halitamdai fedha hizo na badala yake zitatumika kuwa ni rambirambi za kifo chake na pasi yake ya kusafiria itarejeshwa.

xvii. Rambirambi

a. Michango ya rambirambi itatoka nje ya mfuko. Aidha, pamoja na michango kutoka kwa wanashirikisho, Kiasi cha rambirambi kutoka kwenye mfuko kitajadiliwa na kupitishwa na Kurugenzi ya Uchumi na Fedha kwa mwanajumuiya wa Jumuiya mwanachama hai.

b. Rambirambi itatolewa kwa wanajumuiya tu (msiba wa mwanajumuiya) ikishirikisha Jumuiya wanachama zote

c. Jumuiya zote zitashiriki kutoa rambirambi, wahisani na marafiki wa watanzania

d. Misiba ya ndugu wa karibu wa mwanajumuiya itashughulikiwa katika wigo wa Jumuiya na sio shirikisho

e. Rambirambi pia itatolewa endapo aliyewahi kuwa mwanajumuiya na muda wake ukaisha akafariki (TASAFIC Alumni)

**48. Usimamizi wa mfuko**

i. Katika kuhakikisha utekelezaji bora, mfuko utakuwa chini ya usimamizi wa Ubalozi wa Tanzania, Kamati Tendaji na Halmashauri Kuu.

ii. Waweka sahihi wa mfuko atakuwa Mwenyekiti, Mweka Hazina na mjumbe mmoja wa Kurugenzi ya uchumi na fedha atakayeteuliwa na kurugenzi hiyo.

## SEHEMU YA SABA: VYANZO NA USIMAMIZI WA MAPATO

**49. Vyanzo vya mapato ya Shirikisho ni:-**

i. Michango na ada ya kila Jumuiya mwanachama iwe misaada na vyanzo vingine vitakavyobuniwa na kuratibiwa na vikao husika vya Shirikisho.

ii. Shirikisho linaweza kujipatia mali halali zinazohamishika na zisizohamishika na litakuwa na uwezo wa kuchukua, kuhamisha, kuuza au vinginevyo kuondosha mali hizo katika namna itakavyoonekana inafaa.

**50. Usimamizi wa mapato ya Shirikisho**

Usimamizi wa mapato ya Shirikisho utakuwa kama ifuatavyo:–

i. Kamati Tendaji itakuwa na uwezo wa kudhibiti na kusimamia fedha za Shirikisho na uwezo mwingine wowote wa kiutendaji kadiri itakavyokuwa muhimu kwa utekelezaji sahihi wa madhumuni ya Shirikisho.

ii. Malipo yote ambayo hayakupangiwa bajeti yatahitaji uthibitisho wa jumuiya wanachama kwenye mkutano mkuu wa dharura.

iii. Hati zote za malipo zitaidhinishwa na watu watatu kwa pamoja Mwenyekiti, Mweka hazina wa Shirikisho na Mjumbe mmoja wa Kurugenzi ya fedha na uchumi atakaeteuliwa na kurugenzi hiyo. Iwapo Mwenyekiti hayupo, kamati tendaji itamteua kiongozi miongoni mwao kuidhinisha kwa niaba ya Mwenyekiti.

iv. Mweka Hazina ataweka vitabu vya hesabu za Shirikisho katika hali nzuri na atatayarisha maelezo ya Shirikisho na kuwasilisha taarifa ya fedha kwenye kamati tendaji na mkutano mkuu.

v. Mwaka wa fedha wa Shirikisho utaanza mwezi Julai na kumalizika mwezi Juni wa kila mwaka.

**51. Kanuni za usimamizi wa fedha za Shirikisho**

i. Kutakuwa na Kanuni ndogo ndogo za usimamizi wa fedha za Shirikisho kama zitakavyoundwa na kurugenzi ya Uchumi na fedha kwa kila mwaka wa fedha.

ii. Kanuni hizi zitapitishwa na Mkutano Mkuu kwenye kundi sogozi kwa notisi ya siku tatu,kwa kura ya ndio au hapana.

## SEHEMU YA NANE: MASHARTI MAALUMU

### 52. Akidi za Vikao

i. Vikao vya Shirikisho vitaendeshwa na kupitisha maamuzi yoyote yanayohusu Shirikisho endapo idadi ya wajumbe waliohudhuria itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe wote.

ii. Akidi itazingatia hali ya uhai wa shirikisho.

### 53. Ufikiwaji wa maamuzi

i. Katika mikutano yote uamuzi utafikiwa kwa makubaliano ya jumla, au kwa wingi wa kura za wajumbe waliohudhuria na kupiga kura, isipokuwa tu mabadiliko ya kubadili Kanuni yote ya Shirikisho yatahitaji kura ya theluthi mbili ya wajumbe wote waliohudhuria.

ii. Mikutano itaamuliwa mahali pa kufanyika kwa pamoja na Jumuiya wanachama bila upendeleo wowote.

iii. Kwa utaratibu wa bahati nasibu, eneo la mkutano litaamuliwa bila kuweka upendeleo

### 54. Lugha ya Mikutano

i. Lugha ya mikutano yote ya kawaida ya Shirikisho itakuwa ni Kiswahili ili kukuza na kudumisha utamaduni wa Tanzania.

ii. Endapo kutatokeea kutoelewana kwa lugha ya mkutano, lugha nyingine itahitajika ili kuleta ufahamu wa jambo husika, lugha nyingine yoyote inaweza kutumika kwa ajili ya ufafanuzi au uelewa wa jambo hilo.

## SEHEMU YA TISA: UKOMO WA SHIRIKISHO

### 55. Sababu za ukomo wa Shirikisho

Shirikisho litakoma kuwepo endapo kutatokea mgogoro mkubwa na kushindikana kutatuliwaau kusuluhishwa.

### 56. Hatua baada ya kukoma kwa Shirikisho

Endapo Shirikisho litakufa:-

i. Mkutano Mkuu utaitishwa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

ii. Mkutano Mkuu utatoa maamuzi ya mwisho ikiwemo kulipa madeni ambayo Shirikisho linadaiwa au kudai madeni ambayo Shirikisho linadai.

iii. Mali zilizobaki baada ya madeni kulipwa zitagawanywa kwa Jumuiya wanachama haiwote kwa usawa kupitia Mkutano Mkuu.

## SEHEMU YA KUMI: MAKOSA NA ADHABU

### 57. Makosa ya udanganyifu na kutoa taarifa za uongo

i. Jumuiya mwanachama itakayothibitika kutoa taarifa zisizo sahihi juu ya jambo linalopelekea mwanajumuiya wake kuchangiwa kiasi cha fedha kutoka katika Shiriko, Jumuiya hiyo italipa fedha zote alizojipatia mwajumuiya wake na itatozwa faini ya asilimia hamsini ya fedha zote zilizotolewa.

ii. Mwanajumuiya atakayethibitika kutoa taarifa za uongo katika jumuiya yake na kupelekea kujipatia kiasi cha fedha ama kutoka katika jumuiya au katika Shirikisho, jumuiya husika itamuwajibisha kutokana na udanganyifu huo kwa kumuamuru kurejesha fedha yote aliyojipatia pamoja na faini ya nusu ya fedha hizo na adhabu nyengine yoyote kama itakavyoamuliwa na Jumuiya au Shirikisho.

iii. Matumizi mabaya ya fedha za ndani ya Jumuiya na Shirikisho kwa sababu ya uongo iliothibitika bila shaka.

iv. Kutoa maelezo kwa maandishi yenye uongo ndani yake kwa lengo la kupotosha.

### 58. Makosa ya matumizi mabaya ya fedha

**A.** Kiongozi yeyote ambaye, isipokuwa kama yupo katika utekelezaji wa majukumu yake ya kazi moja kwa moja au vyenginevyo kwa yeye mweyewe au kwa mtu mwengine yeyote, katika namna yoyote ile;

i. Anatumia vibaya fedha au mali zozote za Shirikisho.

ii. Anatoa au kuchukua uamuzi kinyume na Kanuni hizi. iii. Anatumia madaraka yake kinyume cha matakwa ya Kanuni hii.

iii. Anatumia vibaya madaraka aliyopewa kwa kuwadhalilisha wanajumuiya wengine, atakuwa ni mkosa na atakapotiwa hatiani atapewa adhabu kama itakavyoamuliwa naHalmashauri Kuu.

iv. Kutokutii maagizo ya Kamati tendaji.

v. Kutokuitikia wito wa Kamati tendaji au halmashauri kuu.

**B.** Adhabu

i. Karipio la mdomo.

ii. Karipio la maandishi kutoka kwa Halmashauri kuu na mlengwa atapaswa kujibu na kupokea karipio.

iii. Kufutiwa uanachama wake ndani shirikisho na kubaki na uanachama wa jumuiya.

iv. Kuvuliwa nafasi yake ya uongozi

v. Jumuiya yake kuvuliwa uanachama ndani ya shirikisho.

vi. Mwanachama/Jumuiya itakayovuliwa uanachama itatengwa kwa muda wa miakamiwili na kuruhusiwa kujiunga tena kwa barua ya maombi.

vii. Adhabu hizi zitaenda kwa kosa lolote lile kulingana na maamuzi ya Kamati tendajipamoja na Halmashauri kuu.

viii. Kila chombo cha maamuzi kitahukumiwa na chombo kilichopo juu yake.

ix. Endapo viongozi wa juu wa shirikisho watahusika kwenye makosa watapaswa kupisha uchunguzi kwa kuitisha Halmashauri kuu na wajumbe kuchagua nani akaimu nafasi,na endapo watapatikana na hatia watahukumiwa kwa mujibu wa kanuni hizi.

x. Hukumu ikimuondoa kiongozi wa Shirikisho, Halmashauri kuu itaitisha uchaguzi ndani ya mkutano mkuu kujaza nafasi zilizo wazi.

xi. Kiongozi atakaye patwa na hatia hatajishughulisha na masuala ya Shirikisho kwa awamu tatu.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA: MAREKEBISHO YA KANUNI

### 59. Idhini ya Marekebisho ya Kanuni

i. Kanuni hizi zinaweza kufanyiwa mapitio wakati wowote, na zinaweza kufanyiwa marekebisho na Kamati maalum ya Sheria na Katiba itakayoundwa na Halmashauri Kuu kwa utekelezaji bora wa Kanuni hizi.

ii. kamati itakusanya maoni na kuyawakilisha kamati tendaji.

iii. kamati tendaji itaunganisha na kuandaa nakala ya mwisho na kuwapa wajumbe wamkutano mkuu wiki moja kabla ili kuipitia.

### 60. Marekebisho ya kanuni za Katiba hii

i. Marekebisho yatapitishwa na Mkutano Mkuu kwa ajili ya kuanza kutumika na nakala kusambazwa kwa Sekretarieti.

ii. Vifungu vitapitishwa kimoja baada ya kingine kwa kura ya ndio au hapana.

iii. Vifungu ambavyo havitapitishwa, vitarekebishwa hapo hapo na kupitishwa au kutopitishwa kwa kupigiwa kura.

iv. Baada ya marekebisho, Kanuni zitasainiwa na Mwenyekiti wa Kamati Tendaji pamoja na Mlezi (Nakala laini na ngumu)

---

**MWISHO**